**Noa Bongo! Jenga Maisha Yako !**

**Utandawazi : Uhamiaji wa Ndani Afrika**

**Autor : Sismons Bidjocks**
**Redaktion : Yann Durand**
**Übersetzung : Anne Thomas**

---

**3 Stimmen : Sauti 3**

- **junger Sprecher 1……..Msimulizi wa kiume 1**
- **junge Sprecherin 1……..Msimulizi wa kike 1**
- **Sprecher (in) 2…………. Msimulizi wa kike 2**
- **als Off- Stimme für die Reportage**

- **Für die O-Ton dazu 1 junger Mann ….Kijana I wa kiume…**

---

**Vorspann LbE………………………….Kiashirio cha Kipindi**

**SEHEMU YA KWANZA – REPORTAGE: REPOTI**

**Msimulizi wa kike 1:** Habari gani !

**Msimulizi wa kiume 1:** Natumai nyote hamjambo ! Leo katika mfululizo wa vipindi vyetu vya utandawazi tutazungumzia juu ya uhamiaji.

**Msimulizi wa kike 1 :** Tutaelekea kwenye mji mkuu wa Cameroon …Yaounde…..

**Msimulizi wa kiume 1 :**

…….hapo tutakutana na mtu anayetokea Ivory Coast….

**1.Globalisierung Binnenmigaration Atmo 1 (unterlegen)………**

**Msimuizi wa kiume 1 + Msimulizi wa kike 1 :**

Kwa hiyo fungeni mikanda tayari kwa safari!

**Globalisierung Binnenmigration Atmo 1 (hoch)**

**Msimulizi wa kike 2 :** Ibrahim Traore ana umri wa miaka 20 tu lakini tayari anamiliki kampuni ya usafiri wa taxi mjini Yaounde.Awali alikuwa akitaka kuhudhuria Chuo cha Cameroon Militaire Inter-Armes ambacho ni chuo cha maafisa wa kijeshi. Hakufanikiwa kuingia kwenye chuo hicho na ilibidi arudi nyumbani Ivory Coast lakini alirudi tena Cameroon kuanzisha biashara ya usafiri wa taxi.

**O-Ton Utandawazi Binnenmigration 1**

Hatimae nilifanikiwa juu ya kwamba mara ya kwanza nlikuwa sikuweza kupata mkopo wowote ule.Baada ya siku,wiki, miezi chungu nzima niliweza kukusanya fedha nyingi kidogo na hivyo ndivyo hatimae nilivyoweza kuanzisha biashara yangu mwenyewe.

**Msimulizi wa kiume 1 :**

Lakini hufikiri kwamba ni hatari kidogo kutumbukiza kila kitu kwa kubahatisha kwenye biashara ya usafiri wa taxi ?

**Msimulizi wa kike 1 :** Kusema kweli ni uamuzi wa busara …..katika baadhi ya nchi za Afrika magharibi kama vile Burkina Faso,Benin au hata Ivory Coast usafiri wa taxi umekuwepo kwa miaka 15 lakini sio Cameroon ambapo huduma hiyo ndio kwanza imeanza hivi karibuni.

**Utandawazi   Binnenmigaration Atmo 2………………..**

**Msimulizi wa kike  2 :** Ibrahim anaanza siku yake saa kumi na mbili asubuhi ambapo huamshwa na sauti za ingini na honi za magari.Katika kituo cha Mimboman …wilaya iliochangamka mjini Yaounde kila mtu hapo humuita kuwa ni Muaivoria.Hapa ndipo

alipoanza kufanya kazi kama mkusanyaji nauli kwa miaka miwili iliopita.

**Utandawazi Binnenimagration Atmo 2 (wieder hoch)………**

**O-Ton Utandawazi Binnenmigtation 2 …………………..**

Lazima nikiri kwamba kwanza haikuwa rahisi …hususan kwa kuwa nilikuwa kwenye nchi mpya na kwa sababu nimeamuwa kufanya biashara ya usafiri wa taxi.Ilinibidi nijerekebishe kwa kuambatana na hali niukumbatie ile nafsi yenyewe ya Wacameroon ambao tayari walikuwa wakiifanya kazi hiyo kwa muda mrefu.

**Msimulizi wa kike 2 :** Lakini Ibrahim alijumuika nao kwa haraka sana hususan kutokana na mambo mawili …alikuwa hodari katika kujiambatanisha na kitu na alikuwa hakukabiliwa na kikwazo cha lugha tafauti na ilivyokuwa kwa wahamiaji wengine wengi.

**O-Ton Utandawazi Binnenmigration 3……………**

Kwenye umma,kwenye miji,katika biashara inatumika lugha ya Kifaransa kwa hiyo nilikuwa sina tatizo kwa sababu tunazungumza Kifaransa nchini Ivory Coast.

**Utandawazi Binnenmigration Atmo 3 Ziegen …………**

**Msimulizi wa kike 2 :** Ibrahim alitaka kuondoka Cameroon kwa sababu ya familia yake ……alikuwa hakutaka kuwa na maisha kama ya wazazi wake ambao walikuwa ni wakulima.

**O-Ton Globalisierung Binnenmigration 4**

Walikuwa ni wakulima ambao mara nyengine ilibidi walime ili waweze kubakia hai yaani waweze kula. Hulima muhogo kidogo ,njugu nyasa na nafaka.Miaka yangu ya mwanzo niliitumia nikiwa kijijini na baadae nilikwenda Abidjan kwa ajili ya kuhudhuria shule.Huko ndiko nilikotumia takriban muda wangu wote hadi pale nilipopata cheti changu cha kumalizia shule.

**Msimulizi wa kike 2 :** Na kuanzia hapo Ibrahim akaanza kufunga safari yake ya kubahatisha .Wakati vijana wengi wa Kiafrika wangelifanya kila linalowezekana kuingia Ulaya kutafuta maisha bora Ibrahim alifikiri kwamba unaweza kufanikiwa kupata unachokitafuta katika nchi jirani yako.

**O- Ton Globalisierung Binnenmigation 5………..**

Ni kweli kwamba katika fikra inayokubalika na wengi …ilio mashuhuri furaha iko katika upande wa pili wa uwa. Sisemi kwamba hilo sio sahihi lakini pia sisemi kwamba hilo ni sawa ingawa sikuwahi kuwa huko kabla.Nafikiri maisha inabidi yaongozwe pale mahala mtu anapokuwepo na kwa kuamini hili niliweza kuendeleza kitu fulani ambacho leo hii kimekuwa thabiti.Lengo langu kuu la kwanza ni kuwa mahala kwengineko na kufanya kitu ambacho kitaniwezesha kuwa imara katika maisha aidha iwe Ulaya au Afrika.Kwa hiyo leo niko Cameroon na niko furahani.

**Msimulizi wa kike 2 :** Kila dereva wa Ibrahim hupata faranga za CFA sarafu inayotumiwa na makoloni ya zamani ya Uafaransa 1,500 kwa siku na huwa wanampatia yeye faranga 3,500 za mapato wanayoyaingiza.Wakati wa jioni wote huwa wanakutana kuzungumzia mipango yao ya siku ya pili.Licha ya mafanikio yake ya hivi sasa Muaivoria huyo wa Mimboman bado ana malengo makubwa zaidi.

**O-Ton Globalisierung Binnenmigartion 6…….**

Ningelipenda kutanuka zaidi kadri inavyowezekana.Lakini sipangi kubakia hapa katika biashara ya usafiri taxi.Ikiwa nitapata fursa ningelipenda kupanda ngazi juu zaidi na kuingia biashara ya usafiri wa taxi jijini Yaounde kwenyewe.

**Globalisierung Binnenmigration Musik (Francis Bebey/ Guitar Makossa 4000617000) unterlegen……………….**

**Msimulizi wa kike 2 :** Tokea alipoondoka Ibrahim amewahi kurudi Ivory Coast mara moja tu.Lakini ameweza kuweka uwiano katika maisha yake.

**O-Ton Globalisierung Binnenmigration 7**

Mimi ni raia wa dunia.Niyumbani ni popote pale ninapojisikia vizuri.Kwa hiyo hapa nilipo Cameroon kwa wakati huu ni nyumbani.Najisikia vizuri tu.Sina ninachokijutia isipokuwa pengine masafa yalioko kati yangu na familia yangu nchini Ivory Coast.

**Musik wieder hoch………………**

**MWISHO WA SEHEMU YA KWANZA**

---

**SEHEMU YA PILI …………  ERKLÄRSTÜCK**

**Msimulizi wa kiume 1 + Msimulizi wa kike 1 tu !**

**Msimulizi wa kiume :** Hamu ya mtu kutamani nyumbani lazima itakuwa ina uma sana ! Lakini na kwa nini mtu aondoke kwao ?

**Msimulizi wa kike :** Unajuwa kwa ujumla wahamiaji wanakuwa hawana chaguo kubwa.Mara nyengine wanakuwa hawana hata rasilmali za kuweza kukidhi mahitaji yao nyumbani…….huu ndio unaoitwa uhamiaji wa kiuchumi…..lakini kuna wakati inabidi wakimbie kwa sababu ya kuwepo kwa hatari ya aina fulani…..

**Msimulizi wa kiume :** ………kama vile vita au ukandamizaji ?

**Msimulizi wa kike :** Ndio hasa……huu unaitwa uhamiaji wa kisiasa.Lakini inazidi kuwa vigumu kutambuwa sababu kwa nini watu wanaamuwa kuhama.Mara nyingi inakuwa ni mchanganyiko wa mambo….

**Msimulizi wa kiume :** Pia majanga ya asili ?

**Msimulizi wa kike :** Ndio kwa mfano kuenea kwa jangwa,ukame,mafuriko, matetemeko ya ardhi……..

**Msemaji wa kiume :** Lakini wahamiaji hawa wote huwa wanatoka wapi ?

**Msimulizi wa kike :** Kwa mujibu wa takwimu za hivi karibuni kabisa wengi wa watu milioni 191 wa dunia ambao wameishi nje ya nyumbani kwao kwa asili ni Waafrika …wanawake wa Afrika ….nusu ya wahamiaji duniani ni wanawake.

**Msimulizi wa kiume :** Kwa hiyo wengi wanatokea Afrika lakini huwa wanakwenda wapi?

**Msimulizi wa kike :** Aidha katika nchi nyengine inayoendelea au kwenye nchi ilioendelea.Ni kama nusu kwa nusu hivi.

**Msimulizi wa kiume :** Kwa hiyo kimsingi ku na watu wengi wanaohamia kutoka nchi za kimaskini kwenda nchi nyengine za kimaskini na wengine wanatoka nchi za kimaskini kwenda nchi za kitajiri na kuna wale wanaotoka nchi za kitajiri kwenda nchi nyengine za kitajiri?

**Msimulizi wa kike :** Ndio ni sawa! Huu unaitwa mmiminiko wa uhamiaji! Wahamiaji wawili kati ya watatu wanaishi katika nchi ya kitajiri.

**Msimulizi wa kiume :** Hii kidogo inachanganya akili!Nimesikia kwamba mmiminiko wa uhamiaji yaani idadi ya watu wanaondoka katika nchi zao za asili inaongezeka kwa asilimia mbili kwa mwaka.

**Msimulizi wa kike :** Hilo pia ni kweli …..na kwa kiasi fulani hutokana na kongezeka kwa wahamiaji wenye ujuzi wa kitaaluma takwimu hiyo imeongezeka maradufu katika kipindi cha miaka ishirini.Haya ni mojawapo ya matokeo mazuri ya utandawazi.

**Msimulizi wa kiume :** Lakini huu pia huitwa kuwa unyonyaji wa wataalamu!Na hilo ni tatizo kwa nchi fukani za kimaskini ambazo zinahitaji wataalamu wenye ujuzi  ili kuweza kuendelea!

**Msimulizi wa kike :** Nakubaliana na wewe lakini tunapaswa tusisahao kitu kimoja hapa ……….kwamba wahamiaji aidha wawe na ujuzi wa kitaaluma au hawana wote huwa wanatuma pesa nyumbani.

**Msimulizi wa kiume :** Ni kweli lakini haliwezi kuwa donge nono!

**Msimulizi wa kike :** Utashangaaa…….katika ngazi ya dunia kima cha fedha wahamiaji wanazowatumia familia zao kimeongezeka kwa wingi sana.Ilikuwa dola za Kimarekani bilioni 105  hapo mwaka 1995.  Miaka kumi baadae kima hicho kilikuwa dola bilioni 232!

**Msimulizi wa kiume :** Doh ! Na bado kwa wastani wahamiaji ndio wenye kuathirika zaidi na ukosefu wa ajira…….

**Msimulizi wa kike :** Ni kweli hususan wale ambao hawana ujuzi mkubwa.Baadhi ya nchi za Ulaya hivi sasa zimekuwa zikichaguwa wahamiaji wa kuwaingiza……..huruhusu wale wenye taaluma ambao wanaweza kufanya kazi katika sekta ambapo wafanyakazi wanakuwa wanahitajiwa sana.

**Msimulizi wa kiume :** Kwa hiyo kwa kadri utakavyokuwa na ujuzi mkubwa zaidi ndivyo inavyokuwa rahisi zaidi kufanikiwa nchi za nje……

**Abspann………………..Funga Kipindi……………**

**Msimulizi wa kike 2 :** Na hapo ndio tumefikia mwisho wa kipindi chetu Noa Bongo! Jenga Maisha Yako!Asante kwa kusikiliza kipindi hiki juu ya utandawazi na uhamiaji wa ndani ya bara la Afrika.Ni kipindi cha Deutsche Welle kilichotayarishwa na Sismondi Bidjocka na Yann Durand.Ili kujuwa zaidi au iwapo unataka tena kusikiliza kipindi hiki nenda kwenye tovuti yetu www.dw-world.de/be
Usikose kujiunga nasi tena mara nyengine.
Kwaheri !